


OFISI YA BUNGE

Jimbo la Bumbuli,
S. L. P. 47,
Lushoto. Bumbuli.

Kumb. Na. MB/GC/1/25

11 Mei, 2010

Katibu wa CCM wa Wilaya,
Ofisi ya CCM ya Wilaya,
S. L. P. 34,
LUSHOTO.



YAH: HOJA YA KUHUFUJUMIWA KISIASA MBUNGE WA JIMBO LA BUMBULI.

Utakumbuka kwamba nilikuandikia barua **Kumb. Na. MB/GC/1/24** ya tarehe 18 Februari, 2010 ikihusu hoja hii hapa juu.

2. Toka wakati huo sasa ni karibu miezi mitatu sijapata majibu yoyote kuhusu hoja hii. Nadhani unakumbuka kwamba kwenye kikao cha mwisho nilichohudhuria cha Kamati ya Siasa ya Wilaya iliamuliwa kwamba nipatiwe majibu kuhusu hoja hii. Aidha, iliagizwa kwamba barua iliyoandikwa na Bwana Leonard Kaoneka ambaye alichukua jukumu la kunishutumu na ambayo ilisomwa mbele ya Halmashauri Kuu ya CCM ya Wilaya ichambuliwe na mimi nijulishwe kwamba alikuwa anaandika shutuma zake akiwa na wadhifa gani. Hii ni muhimu maana ni wazi alikuwa na yeye anapiga Kampeni hadi kuwashitaki Afisa Tarafa wa Bumbuli na Afisa Mtendaji wa Kata ya Bumbuli kuwa Wahamishwe maana hawakumpa msaada katika Kampeni zake. Naona agizo lake la Afisa Mtendaji wa Kata kuhamishwa limetekeleza. Hivi LEONARD KAONEKA anawadhifa gani unamuwezesha kuagiza mambo na yakatekelezwa?

3. Kwa kutekeleza utawala bora na demokrasia naomba nipatiwe nakala ya barua ya Kaoneka maana inahoja ambazo zimenitia kichefuchefu na hapana budi nimchukulie hatu za Kisheria.

4. Kwa upande mwingine, kama niliyoeleza katika barua yangu niliyo nukuu hapo juu, Kampeni za Januari Makamba zilianza tarehe 3 Septemba, 2009 kwa hiyo zimekuwa zikiendelea kwa muda wa miezi tisa (9) sasa bila wasiwasi kama ifuatavyo:-

4.1 Tarehe 4 April, 2010 zilifanyika Kampeni katika Kata ya Vuga na Mgwashi:

- (a) Kata ya Vuga Kampeni ilifanyika asubuhi saa 4 hadi saa 9 mchana. Yalitumika Mabasi Madogo Matatu (3) yaliyotaka Watu kutoka Mbuzil, Soni na Vuga. Mkutano huo ulifanyika Vuga - Kitali. Walioshiriki: Januari Makamba, Shabani Bosinia Shekilindi, Ramadhani Mahanyu na Wapambe wa wengine. Ujumbe wao ni kwamba wameamua kuenda kila PASAKA na Wananchi wa Vuga. Pilau na Vinywaji vilitolewa na ahsante za fedha.
- (b) Kata ya Mgwashi Kampeni ilifanyika jioni na Muandaji ni Bwana Immam Kibai Shemhaka, Mwenyekiti wa CCM wa Kata. Walikunywa Wananchi wawiliwawili kutoka Matawi yote ya Kata ya Mgwashi. Kampeni ilihitimishwa na takrima ya Chakula, Vinywaji na ahsante ya fedha kwa kila aliyehudhuria. Washiriki walikuwa Januari Makamba, Shabani Bosinia Shekilindi, Ramadhani Mahanyu na Wapambe wa Mgwashi. Kikao kilifanyika Nyumbani kwa Mama MVUNILWA, Mama Mkwe wake Mwenyekiti wa CCM wa Kata aliyehandaa Mkutano huo.
- Walitumia Magari haya:-

- (i) T.548 AZG la Januari Makamba,
- (ii) T. 568 AWP la Mfanyabiashara Shabani Bosinia Shekilindi.

4.2 Tarehe 5 April, 2010 Kampeni ilifanyika Kata ya Mpande na utaratibu ni ule ule wa kukusanya Wananchi kutoka kwenye Matawi. Mkutano ulifanyika kwenye eneo la Nyumba ya Mfanyabiashara David Shemakange. Chakula na ahsante ya fedha ilitolewa. Walioshiriki ni Januari Makamba na Shabani Bosinia Shekilindi.

- Magari yaliyotumia ni T. 548 AZG la Januari Makamba na T 568 AWP la Shabani Bosinia Shekilindi.

Tarehe 6 Aprili 2010 Kampeni ilifanyika Kata ya Bumbuli katika eneo la Nyumba ya Mfanyabiashara Najim Msenga. Utaratibu ni ule wa kuita Wananchi wawiliwawili kutoka Matawi yote ya CCM ya Kata ya Bumbuli. Vyakula, Vinywaji na ahsante za fedha

baada ya Mkutano. Washiriki walikua Januari Makamba na Mfanyabiashara Najim Msenga na Wapambe wao wa Bumbuli.

- Gari T.548 AZG la Januari Makamba ndilo liliotumika.

TUKIO BAYA ZAIDI

Katika ziara zao hizi walikuwa na Waandishi wa Habari wa Magazeti ya **Rai** ambao waliandika katika Makala ya tarehe 8 – 14 Aprili, 2010 maelezo ya ovyo dhidi yangu.

Aidha, Gazeti la **Mkakati** la tarehe 9 – 15 Aprili, 2010 nalo liliandika mambo ya uzushi. Zote hizi ni Kampeni chafu kabla ya Uchaguzi. Na zimeandaliwa rasmi. Kwa taarifa yako, WAHARIRI wa Magazeti hayo nimewafikisha kwa Waziri wa Habari, Utamaduni na Michezo maana mambo yaliyoandikwa hayanidhalilishi Mimi tu bali Wananchi watulivu wa Jimbo la Bumbuli na Chama chao CCM. Nashindwa kuelewa wapiga Kampeni hao ni wa Chama gani?

KILICHOFUATA BAADA YA ZIARA HIYO RASMI

Napenda kuweka Kumbukumbu kuwa wakati wa ziara hiyo rasmi ya Januari Makamba akiongozwa na wateuliwa rasmi Ramadhani Mahanyu na Shabani Bosinia Shekilindi nilikuwepo Jimboni wakati huo wa Pasaka maana wanavizia nikiwanje ya Jimbo ndipo hufanya vituko vyao. Nilikuwa kwenye Mikutano ya Kamati za Bunge kuanzia 29/4/2010 hadi tarehe 1/5/2010. Hivyo tarehe 2 Mei, 2010 hadi tarehe 7 Mei, 2010 siku ya Kumbukumbu ya Sheika Abedi Amani Karume nilikuwa Bumbuli.

- 1 Tarehe 22 Aprili, 2010 Ramadhani Mahanyu alikuwa Bumbuli Wema, Kwengeza, Tekwa, kufanya Kampeni. Alifanya Mkutano na Wananchi 20 wakapewa maagizo kwenda kuonana na Mabalozi wa CCM.

Tarehe 25 Aprili, 2010 wafuatao walifika Bumbuli na Milingano kufanya Kampeni na mmoja tu ndiye Mtu wa Bumbuli wengine ni wa Korogwe:

- 5.2.1 Shabani Shechonge
- 5.2.2 Emmanuel Shechambo
- 5.2.3 Ruth Kimweri
- 5.2.4 Saadala Kabado.

Walitumia Gari Na. T 218 AZR HUNDAI

5.3 Tarehe 5 Mei, 2010 Wafuatao wakitumia Gari Na. T 531 AJS Hard Top ikiendeshwa na Dereva Edward Mkukutika wa Wizara ya Maliasili Dar es Salaam ambaye yuko likizo:

- 5.3.1 Rashid Shedafa
- 5.3.2 Juma Kilimo
- 5.3.3 Martin Zaakuu
- 5.3.4 Iddi Guga
- 5.3.5 Rogate Teme
- 5.3.6 Hamida Kizokwa
- 5.3.7 Abdallah Zahabu Mchuzi,

Walikwenda Mayo, Kwabosa, Kisiwani na Shembekeza kufanya Kampeni na kugawa Simu aina ya Nokia zenye Tochi 50 kwa nia ya kuwashawishi Wananchi wamchague Mgombea wao Januari Makamba.

5.4 Tarehe 8 Mei, 2010 wafuatao wakiwa na Pikipiki zifuatazo:-

- (a) T. 552 AYL ikiendeshwa na Joseph Gendo na
- (b) T. 207 AUR ikiendeshwa na Khalidi Shenkome, walikwenda Funta, Balangai, Mpalalu na Tekwa kufanya Kampeni. Walifuatana na Wanafunzi Wawili wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM).
- (i) Immanuel Sanga na
- (ii) Henry Stambuli.


Wanafuzi hao ambao siyo wenyeji wa Bumbuli wametoa Ujumbe kuwa wenzao Chuo Kizima wanamuunga mkono Januari Makamba.

5. Bwana Katibu wa Chama cha Mapinduzi wa Wilaya ya Lushoto nimeyaandika haya yote ili ujue nini kinatendeka Bumbuli. Wewe huwezi kuyajua na sasa ni miezi 9 Kampeni za Januari Makamba zinaendelea bila wasiwasi. Sasa ninachouliza ni kwanini na wale Wanachama wengine waliotangaza nia ya kugombea Ubunge Jimbo la Bumbuli nao wasiruhusiwe kufanya Kampeni?

Napenda kukumbusha tu kuwa tuko kwenye mfumo wa Siasa ya Vyama vingi. Vyama vingine vinatuangalia tu tunayofanya.

7. **SWALI:** Kwa nini Kampeni Jimbo la Bumbuli zinaongozwa na Watu wa Jimbo la Lushoto – Shekilindi na Mahanyu? Wenyewe wa Bumbuli hawatoshi?
8. Sitaandika tena, haya ni maandishi yangu ya mwisho kuhusu yanayofanyika Bumbuli na naona ni vema ngazi za juu zielewe hii.

Nakushukuru kwa ushirikiano wako.


W. H. Shellukindo (Mb)
Mbunge Aliyeko Madarakani.

Nakala kwa : Mhe. George H. Mkuchika (Mb)
Naibu Katibu Mkuu wa CCM,
Makao Makuu ya CCM
S. L. P. 50
DODOMA. Kwa taarifa

Bw. Muba,
Katibu wa CCM wa Mkoa,
Ofisi ya CCM ya Mkoa wa Tanga,
S. L. P 2070,
TANGA. Kwa taarifa.